

# \*Mifugo 25,000 kuvishwa hereni za kielektroniki

**Arusha**

**NA LILIAN JOEL**

**H**ALMASHAURI ya Arusha iliyopo wilayani Arumeru mkoani hapa, inategemea kuanza utambuzi wa mifugo 25,000 kwa awamu ya kwanza ikiwa ni utekelezaji wa agizo la serikali la kuvisha mifugo hereni za kielektroniki.

Akizungumza jana wakati wa kupokea hereni hizo kutoka Kampuni ya S&J, Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Arusha, Dk. Yohana Kiwone, alisema uvishaji hereni mifugo hiyo utaanza mara moja ambapo lengo ni kuvisha mifugo yote iliyopo katika halmashauri hiyo.

Kwa mujibu wa Dk. Kiwone katika Halmashuri ya Arusha, utambuzi utafanyika kwa awamu nne ambapo jumla ya mifugo 200,019, inategemea kuvikwa hereni hizo za kielektroniki wakiwemo ng'ombe 81,550, punda 3,535, mbuzi 60,671 na kondoo 54,245.

*Aliwataka wafugaji wote wa halmashauri*

hiyo kuwa tayari kutekeleza agizo hilo ka serikali la kuvika mifugo yao hereni za kielektroniki kwa kutoa ushirikiano kwa maofisa mifugo.

"Naomba kila mfugaji atoe ushirikiano, msifice mufugo yenu na kila mfugaji atagharamia hereni za mifugo yake kwa mifugo itakayoainishwa awamu hii ya kwaza. Gharama ng'ombe na punda ni sh. 1,750 na gharama ya mbuzi na kondoo itakuwa sh. 1,000 kwa kila mifugo mmoja, hivyo wafugaji wote wanapaswa kujitokeza katika maeneo yao," alisema.

Dk Kiwone alitaja faida za uwekaji hereni hizo za kielektroniki kuwa ni kutambua mifugo kulingana na umiliki na eneo inapotokea, kidhibiti wizi wa mifugo na magonjwa, kuimarisha soko la ndani na nje la bidhaa za mifugo pamoja na kutatua changamoto ya migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

"Uwekaji huu wa hereni utakuwa na tija kwa serikali pamoja na wafugaji kwa sababu tutajua idadi halisi ya mifugo, nani anaimiliki na iko sehemu gani, lakini pia itatusaidia

kuimarisha masoko ya mazao ya mifugo ndani na nje ya nchi," alisisitiza.

Kwa upande wake, mfugaji kutoka Kata ya Oldonyosambu, Loishiye Mollel, alisema wanaishukuru serikali kwa kuanzisha mpango huo kwa kuwa utasaidia kujua idadi halisi ya mifugo na kila mfugaji atajulikana anamiliki mifugo aina gani.

"Tuko tayari kutoa ushirikiano kwa serikali, nitoe rai kwa wafugaji wenzangu kujitokeza kwa wingi kulipia hereni za mifugo anayomiliki hali ambayo itasaidia serikali kujua idadi halisi ya mifugo na kupanga bajeti kwa uhalisia katika sekta ya mifugo," alibainisha.

Utambuzi wa mifugo kwa njia ya kielektroniki unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji ya Mwaka 2012, inayoelekeza kutumia hereni za kielektroniki na taarifa za mifugo na mfugaji zitachukuliwa katika nakala ngumu na nakala za kielektroniki kisha kuingizwa kwenye kanzi data ya taifa.

UOKOAJI Katika Wilaya  
bazo hazina huduma hiyo.

NIPASHE UK 10.

# Mashamba madume bora ya ng'ombe kuimariswa

MBUNGE wa Bahi (CCM), Kenneth Nollo, amehoji mpango wa serikali wa kujenga kituo cha uzalishaji wa madume bora ya ng'ombe wilayani Bahi ili kuleta tija kwa wafugaji na kukidhi mahitaji ya soko.

Ikijibu swali hilo bungeni jana, Wizara ya Mifugo na Uvuvi il-isema mpango wa serikali ni kuimariswa mashamba yake ya uzalishaji wa madume bora ya Mabuki - Mwanza, Kitulo - Njombe na Sao Hill lililoko mkoani Iringa ili kuzalisha madume mengi na bora kwa lengo la kuyasamba-za kwa wafugaji wote wanaohitaji ikiwa ni pamoja na wafugaji wa Wilaya ya Bahi.

Pia ilisema serikali inaendelea kusisitiza matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji katika kuboresha kosafu za ng'ombe ili kuwa na kundi la mifugo yenye tija katika uzalishaji wa nyama au maziwa na hivyo kukidhi mahitaji ya soko.